



## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

### TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU KUANZA KWA MAFUNZO YA WAKUFUNZI WA SENA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022, NGAZI YA MKOA TAREHE 06 JULAI, 2022

*Ndugu Wanahabari,*

Kama mnavyofahamu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea na maandalizi ya Sena ya Watu na Makazi ambayo itafanyika tarehe 23 Agosti 2022. Kwa mujibu wa miongozo ya Umoja wa Mataifa ya kufanya Sena ya Watu na Makazi, mafunzo kwa wakufunzi, wasimamizi na makarani wa Sena ni hitajio la msingi katika kufanya Sena yenye ubora na inayokidhi vigezo vya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

*Ndugu Wanahabari,*

Mafunzo katika ngazi ya Taifa yamekamilika na yalifanyika kwa siku 21 kuanzia tarehe 10 hadi 30 Juni, 2022. Lengo la mafunzo haya lilikuwa ni kuwajengea uwezo na uelewa wa pamoja washiriki wote kuhusu nyenzo zote za sena pamoja na utaratibu mzima wa kufanya Sena ya Watu na Makazi, Sena ya Majengo na Sena ya Anwani za Makazi ili waweze kwenda kufundisha katika ngazi ya Mkoa.

Washirikiri wa mafunzo katika ngazi ya Taifa walikuwa ni Wataalam kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, wawakilishi kutoka Vyama vya Watu wenye Ulemavu na Wawakilishi kutoka Sekta Binafsi na Vyuho Vikuu na vinavyolingana.

*Ndugu Wanahabari,*

Ikumbukwe kuwa, kuanzia tarehe 6 hadi 26 Julai 2022, Kamati za Sensa katika ngazi ya Wilaya, Kata, Mitaa na Shehia watakuwa na jukumu kubwa la kukamilisha mchakato wa ajira za makarani na wasimamizi wote Nchi nzima na kuhakikisha kuwa Makarani wote 205,000 wanatoka katika maeneo wanayoishi.

*Ndugu Wanahabari,*

Kabla sijahitimisha, wito wangu kwa watendaji wenzangu katika ngazi ya mkoa, wilaya, kata, mitaa, na shehia uhakikishe tunafuata utaratibu na kuweka Uzalendo mbele na Busara katika kufanikisha zoezi hili la Kitaifa na Kimataifa hapa Nchini.

*Ndugu Wanahabari,*

Nimalizie kwa kuwashukuru sana kwa ushirikiano wenu na kupitia kwenu ni imani ya Serikali kwamba ujumbe huu utawafikiwa Watanzania wote na kwa pamoja tutakuwa na Sensa ya mafanikio kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Asanteni sana kwa kunisikiliza

Imetolewa na:

Mtakwimu Mkuu wa Serikali,  
Ofisi ya Taifa ya Takwimu,  
Dodoma,  
06 Julai, 2022.

